

# JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA



## OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU WANAFUNZI KURIPOTI SHULENI MWAKA 2023

#### **Dar es Salaam, 12 Januari, 2023**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anapenda kutoa taarifa kwa umma kuhusu hali ya uandikishaji wa Wanafunzi wa Elimu ya Awali na Msingi pamoja na Mapokeo ya Wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa Mwaka 2023. Hadi kufikia leo tarehe 12 Januari, 2023 hali ilikuwa kama ifuatayo;

#### ***1. Maoteo ya Wanafunzi wa Elimu ya Awali***

- Wanafunzi Wavulana ni 2,800
  - Wanafunzi Wasichana ni 2,900
- Jumla ya Maoteo ni Wanafunzi 5,700

#### ***2. Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Awali***

- Wanafunzi Wavulana ni 2,131
  - Wanafunzi Wasichana ni 2,121
- Jumla ya Wanafunzi 4,252 wameandikishwa Elimu ya Awali kwa Shule za Serikali

#### ***3. Maoteo ya Wanafunzi wa Darasa la Kwanza***

- Wanafunzi Wavulana ni 12,600
  - Wanafunzi Wasichana ni 12,800
- Jumla ya Maoteo ni Wanafunzi 25,400

#### ***4. Uandikishaji wa Wanafunzi wa Darasa la Kwanza***

- Wanafunzi Wavulana ni 11,769
  - Wanafunzi Wasichana ni 10,647
- Jumla ya Wanafunzi 22,438 wameandikishwa Darasa la Kwanza kwa Shule za Serikali.

**5. Wanafunzi waliopangiwa Kidato cha Kwanza**

- Wanafunzi Wavulana ni 16,266
- Wanafunzi Wasichana ni 15,559

Jumla yao ni Wanafunzi 31,825

**6. Wanafunzi walioripoti kuanza Kidato cha Kwanza**

- Wanafunzi Wavulana ni 9,515
- Wanafunzi Wasichana ni 9,932

Jumla ya Wanafunzi walioripoti hadi sasa ni 19,447

Aidha, Mkurugenzi anatoa wito kwa Wazazi/Walezi kuhakikisha Watoto wao wanaripoti Shuleni, kwani Muhula Mpya wa Masomo umeanza tangia Tarehe 09 Januari, 2023.

Imetolewa na;



Gatson Leo Makwembe  
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

**OFISI YA MKURUGENZI, 1 MTAA WA MISSION, S.L.P 20950,  
DAR ES SALAAM, SIMU NA 2128800, 2128805, Tovuti: [www.dcc.go.tz](http://www.dcc.go.tz),  
Barua Pepe: [info@dcc.go.tz](mailto:info@dcc.go.tz)**